# NGUVU ZA MUNGU

*Matendo 1:8 "Lakini mtapokea nguvu, akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu nanyi mtakuwa mashahidi wangu katika Yerusalemu na katika uyahudi wote na samaria na hata mwisho wa nchi".*

Hebu na tuone kile nabii wa Mungu amesema juu ya hilo:

Leo tunayo mawazo yasiyo sahihi juu ya nguvu. Nguvu ni kushinda, kurudisha zuri kwa ubaya, hiyo ni nguvu halisi, hiyo ni nguvu ya Mungu (Matayo 5:44-48).

Wendawazimu wanaweza kukata minyororo. Lakini inamchukua mtu halisi kurudisha wema kwa ubaya, kutoka moyoni mwake, siyo kwa sababu ya wajibu wa kidini, bali ni kitu cha moyoni.

Unajua, watu wanataka nguvu, na kwa ukweli hawajui nguvu ni nini, unaona? Hawajui hasa ni kitu gani kinaenda nayo. Njia ya kwenda juu siku zote ni chini. Kama unataka nguvu, angalia vile unavyoweza kujinyenyekesha (Matayo 11:28-30; 1Petro 5:5-6). Ondoka tu kwenye mawazo yako ya ulimwengu na ujinyenyekeshe mwenyewe mbele za Mungu, na hapo sasa utakuwa na nguvu zaidi ya mtu anayekimbia juu ya jengo lote na kufanya kelele nyingi, kwa sababu umejishinda mwenyewe na kujiweka mkononi mwa Kristo ili kujinyenyekesha mbele zake (Yakobo 4:10) Hiyo ndiyo nguvu halisi.

Nionyeshe kanisa lililo nyenyekevu, nyenyekevu hasa, siyo kanisa linalojiona au lenye kiburi; lenyewe ni tamu, kanisa nyenyekevu. Nitakuonyesha kanisa lililo na upendeleo na nguvu za Mungu ndani yake. Hiyo ni kweli. Hicho ndicho kitu kinachohitajika. Unyenyekevu, kujinyenyekeza wenyewe mbele za Mungu, na kumuachia Mungu atende kazi kupitia sisi. Haihitajiki kupiga kelele sana.

Wakati mwingine kama mkulima alivyosema, aliende shambani akiwa na gari lake na kila mara lilipogonga katuta, lilipiga kelele na kuendelea. Lakini aliporudi aligonga vituta vile vile na halikupiga kelele hata kidogo, kwa sababu lilikuwa limejazwa vitu vizuri. Kwa hiyo nafikiri hiyo ni sawa sawa, kwamba tunapojazwa na vitu vizuri vya Mungu, kwamba tunda la Roho lingejulikana kupitia sisi (Wagalatia 5:22).

Sasa Ndugu na dada zangu, napenda kuwauliza jambo fulani kama tumezaliwa mara ya pili kwa Roho wa Mungu ……….. Mungu hana sehemu ndogo dhaifu na sehemu kubwa zenye nguvu. Yeye jumla ni Mungu na kama una Mungu wa kutosha ndani yako, mpaka ingekuwa tu kakivuli, hiyo ni nguvu itoshayo kufanya dunia mpya. Hiyo ni nguvu itoshayo kufanya mwezi mpya na utaratibu mpya. Ni Mungu, na ina nguvu. Na hata sasa ndani ya kila mwamini hapa aliye na uzima wa milele, ambao ni Roho wa Mungu ndani yako, ni nguvu itoshayo kufufua wafu, kuponya wagonjwa, ambayo itafanya mizunguko ya sayari iendelee, lakini inatawaliwa na sheria ambayo ni Roho aliye ndani yako. Ninyi ni wana na binti za Mungu, Roho yule yule ndani yako. Ninyi ni wana na binti za Mungu. Roho yule yule ambaye unaye ndani yako, atakuinua wewe mwenyewe siku ya ufufuo (Rumi 8:11).

Kama hakukuwa na sheria kwa hilo, wana na binti za Mungu wangeweza kuumba dunia yao na kwenda kuishi wenyewe huko. Una nguvu za kufanya hivyo ndani yako. Kama una kakivuli tu ka nguvu za Mungu ndani yako. Una nguvu ya kufanya hivyo. Mungu hashindwi na lolote. Unaona ninachomaanisha? Nguvu zilizo ndani yako zitakufanya ……. Unaweza kunena na dunia ikaumbika na uende ukaishi juu yake Haleluya. Unaona hilo.

Hiyo ndiyo nguvu iliyoko ndani ya Kanisa sasa; Lakini ina tawaliwa na sheria (Waefeso 3:20 – 21) Na sheria hiyo siyo kushika fungu la amri. Ni sheria ya Imani.

Yesu alisema, "Yote yawezekana kwake aaminiye" (Marko 11:22-24). Na kama unaweza kuliamini hilo, chochote Mungu atakachoongoza nafsi yako kuamini, hicho ni chako, Mahali popote nyayo za miguu yenu zitakapokanyaga kwa imani, Mungu anakupa hilo. (Joshua 1:3). Amen itakuwa ni yako. Unaimiliki, kama unaweza kupata ufunguo wa Sheria hiyo ya Imani hiyo inakufungulia unaona ninacho maanisha. Nguvu hizo zinatawaliwa na …………………… Kama wewe ni mwana wa Mungu na binti wa Mungu, hiyo haikuachi kamwe, inakuwa nawe wakati wote. Lakini Imani yako ndiyo inayoenda mbali nayo, lakini yenyewe iko palepale. Haleluya.

Unapookolewa, Mungu anakupa Imani ya kuinuka kutoka kwenye matope ya ulimwengu. Imani yako inashinda mambo ya dunia (1 Yoh 5:4) Imani yako ni nini? Imani yako ni lile tendo la Mungu alilolitenda ndani yako kukufanya mwana wa Mungu, unaacha kusema uongo wako, unaacha wizi wako, unaacha ulevi wako, kwa sababu imani yako inakuinua juu ya hayo. Amina.

Kama hufanyi hivyo, huna imani yoyote. "Na ni kwa imani umeokolewa, na hiyo ni kwa Neema" (Waef. 2:8-9.

Kwa kadiri ya Imani yako uliyonayo (utakayotoa) ndiyo kiasi cha nguvu unazoweza kupata. Kwa sababu ndani yako kuna nguvu za kuumba Mbingu na Nchi. Mungu anakaa ndani yako, na wewe ni Mwana na Binti wa Mungu. Amina. Tuko hapa. Lakini ni imani yako. Yesu alisema "kutokana na imani

yako naiwe kwako kama ulivyoamini". Kama unaweza kuamini, mambo yote yanawezakana. Amin Amin nawaambia, kama utauambia mlima huu, ng'oka na usione shaka ila uamini kile ulichosema……………….

Hiyo ndiyo shida ya Kanisa. Tunaweza tukashinda kila ugonjwa. Tunayo nguvu ndani yetu. Tu wana na binti za Mungu, hakuna kiwezacho kusimama mbele yetu. Jambo moja tu, Anataka kupata mtu fulani ambaye ataiamini, atakayeamini Mungu alishakifanya tayari kwa ajili yako. Siyo tutakuwa, tu hivyo sasa. Na uwepo wa Roho wa Mungu usioshindwa uko pamoja nasi Amina. Tuko hapo.

Amini hilo. Inakupasa kuliamini hilo. Inabidi kuwe na kitu fulani ambacho kitaondoa kikwazo hicho, kufungua kitu hicho ili kukuacha uingie ndani ya hilo. Tunachohitaji leo sio kuomba kwa ajili ya nguvu zaidi, tunayo nguvu itoshayo kufanya Nchi mpya. Unachohitaji ni imani ya kutumia nguvu hizo. Unachohitaji ni kutawala hayo maisha na kuishi maisha yaliyo ya kimungu, kwamba unapomuomba Mungu chochote unajua. Tunakuwa na uhakika na Mungu juu ya hilo. Tunajua kama tunashika amri zake, hatatuzuilia kitu chochote kilicho kizuri. Kama tunatembea naye. Mungu akitembea nasi.

Na nguvu zilezile, Kristo yule yule … Haleluya. Acha hao watu wanaofuata kanuni, watu wanaokana nguvu za Mungu waseme siyo sawa, Lakini nguvu ileile iliyonena na dunia ikaumbika iko ndani ya watu walio na Roho Mtakatifu (waebr. 11:1-3). Hiyo ni kweli, wanaume na wanawake, ni wakati wa kutafuta na kujitambua wewe u nani. Shetani anajaribu kukuficha nyuma, kukuambia wewe ni mdogo – wakukanyagwa chini. Siyo, ninyi ni wana na binti za Mungu (Wagalatia 4:6-7). Uungu hauko Mbinguni, uko ndani yako (Kolosai 1:27) Haleluya.

Mungu anaishi ndani ya watu. Na mtu anakuwa Mwana wa Mungu, siyo kwa uwezo wake mwenyewe, lakini kwa Roho mtakatifu aliye ndani yake ambaye ni Mungu. Muumba akiishi ndani ya viumbe alivyoumba.

Roho Mtakatifu yuleyule aliyewaokoa waluteri, akawatakasa Wamethodist, ambaye aliwabatiza Wapentekoste, sasa hivi anaweka utaratibu wa kuja kwake Bwana Yesu. Hapo ndipo Itakapokuwa na nguvu sana, ule Mwili utakapokuja ndani ya kundi hilo Kanisa, ambayo itawavuta waliobaki watoke makaburini. Kutakuwa na ufufuo. Hiyo ndiyo sababu roho Mtakatifu yuko kwa hilo.

Roho Mtakatifu ni nini? Bila ya sisi hawawezi kukamilishwa
(Waebr. 11:32-40).

Mungu ananisubiri mimi na wewe. Kanisa linakungojea wewe na mimi. Wakati wakufanywa wana, ambapo Mungu anaweza akatumwagia ukamilifu wake, wa nguvu zake, ufufuo wake, kwamba Kanisa na Kristo vimekuwa karibu sana pamoja mpaka kristo awe anaonekana wazi miongoni mwetu na kuinua wafu, na hapo tunaenda kwenye unyakuo (1 Wathes. 4:13-18).

Usiwe na shaka. Mungu anasubiri, na kujaribu kusukuma ili kuzifanya siri za Mungu zifunuliwe katika kanisa lake, hicho ndicho kinachozuia kule kuja kwa Kristo sasa na ule utawala mkuu wa miaka elfu, ni hii nguvu ya kimbinguni, halisi na iliyo kuu iliyotulia bila kutumika. Ndani ya Kanisa.

Ooh, Nguvu ya Kanisa la kikristo iliyolala bila kutumika usiku wa leo kwa sababu ya kutokuamini.

Mnayo nguvu. Lakini imetulia bila ya kutumika, kwa sababu unaogopa kuitumia. Unaona? Wanafunzi walikuwa na nguvu, lakini hawangeweza kulifanya hilo (kumponya yule kijana, Luka 17:20-21). Na kila mmoja wenu ana nguvu. Hawa watu walio vilema sasa hivi wana nguvu ya kuweza kuwainua na watembee. Huyu mtu aliye na kanser (saratani) ana nguvu za kumwinua na atembee. Na ninyi wote mlio wagonjwa pale, mnazo nguvu, mnazo nguvu, mmepewa hizo. Mtapokea nguvu (Matendo 1:8). Hivyo ndivyo Biblia imesema.

Sikilizeni kwa karibu. 1Kor. 4:20 anasema ufalme wa Mungu uko ndani ya neno lake likifanyika nguvu.

Kama unataka kuandika hilo hiyo ni 1Kor. 4:20. Ufalme wa Mungu ni neno la Mungu likifanyika nguvu. Ufalme wa Mungu ni nini? Uko ndani yenu. Ufalme uko ndani yenu (Luka 17:20-21). Neno linapokuja pale, lile neno linaanzisha nini? Linajigeuza lenyewe na kuwa nguvu, inalifanya liseme hasa vile ambavyo limesema.

Huwezi ukasema "Linasema hivyo, Linasema hivi" na kufanya litende kazi. Inabidi useme jambo lile lile ambalo limesema, hiyo inafanya ungamo. Siyo kusema, vyema limeunganishwa kidogo hapa, nitapata maarifa zaidi, nitakuwa na msimamo mzuri juu pale.

Wewe kaa na neno. Liko pale. Unaona? Na inalifanya liwe nguvu. "Yesu Kristo yule jana leo na hata milele" Yesu alisema katika Yohana Mt. 14:12. Yeye aniaminiye mimi , kazi nizifanyazo naye atazifanya". Yohana Mt. 15:7, …. "Mkikaa ndani yangu na maneno yangu yakikaa ndani yenu, Ombeni lolote mtakalo nanyi mtatendewa".

Nguvu hizo za ufufuo, ndugu, simaanishi kitu fulani unachoweza kuchimba na kusukuma na kujaribu. Namaanisha ujiachilie tu mwenyewe, na Mungu tayari amekuchukua mahali fulani mbali kule ng'ambo, ambapo ni furaha kuishi kwa ajili ya Yeye. Hakuna chochote pale ……… kwanini? yale mambo mengine yamekufa kama usiku saa sita. Unaona? Hakuna, hapana shauku tena, hapana hukumu kwa hao walio ndani ya Kristo Yesu ….. Jamani.

Mambo yale ya zamani ya dunia, huna haja ya kuyaacha huna haja, hakuna la kuacha, yenyewe yana kuacha wewe, ni rahisi, hayapo pale tena, yanaenda mbali. Amina.
Nguvu za kuhuisha zimekuja katika siku hizi za mwisho Ni nini? Nguvu za kuhuisha zikija Kanisani, kumfanya mke awe tayari katika saa tunayoikaribia; Nguvu za kuhuisha. Ooh. Mungu tusaidie tuipokee. Tusaidie tuiamini.

Unaona? Inategemea ule mtazamo wako utakaouchukua juu yake ikiwa itakusaidia kukufanyia jambo zuri au hapana hata. Unaona, inabidi uliamini hilo, kama huliamini hilo, haitakufanyia jambo lolote zuri.

Lakini pia ni ukweli kwamba Nabii wa siku za mwisho yupo akileta ujumbe kutoka kwa Mungu ambao utatangulia kule kuja kwa pili kwa Bwana, kwa maana kwa ujumbe wake mioyo ya watoto itageuzwa kuwaelekea mababa wa Pentekoste kule nyuma, na baada ya kurudishiwa Neno kutakuja kurudishiwa Nguvu.

Lakini kanisa halijatambua siku yake, kama Israel aliporudishwa kule kwenye Nchi ya Ahadi nyuma. Hajui alirudije pale nyuma pale. Yeye alirudishwa tu bila kutumia akili yake alirudishwa nyuma pale. Kwa nini? Nguvu za Serikali/Taifa zilimrudisha mahali pake. Nguvu za Kiserikali zitaliweka Kanisa kwenye baraza la Makanisa Duniani. Lakini nguvu za Mungu zitawaweka watu ndani ya Bibi Arusi. Dunia inasukumia upande huu na Dunia inasukumia upande huu, lakini Mungu anasukumia kwenda juu. Roho wa Mungu, ambaye ni Neno la Mungu "(Maneno yangu ni Roho tena ni uzima itamweka Bibi Arusi mahali pake, kwa sababu atatambua mahali pake katika Neno; na hapo atakuwa yuko ndani ya Kristo)"

(Yohana 6:63) itamuweka mahali pake. Hakuna nguvu za Kitaifa/Kiserikali ziwezazo kufanya hilo. Lakini nguvu za kitaifa ziliendesha Israel kwenda kwenye nchi yao nyumbani. Nguvu za kitaifa za Baraza la Makanisa Duniani zitaendesha kila Dhehebu ndani yake, lakini nguvu za Mungu zitaliinua Kanisa Bibi Arusi kwenda utukufuni, mbali na hilo.

Hebu tuchukue Agano jipya, 2Tim. 3:1-5. Roho Mtakatifu ametuonya kwamba siku za mwisho kwamba Kanisa litaondoka kwenye uaminifu na Imani. Watakuwa na mfano wa utauwa, lakini watakana nguvu zinazoenda na vitu sahihi. Wakiwa na mfano wa utauwa; lakini wakikana nguvu zake ndiyo Bwana.

Mungu anachukia dini isiyo na nguvu. Na dini yoyote leo ambayo haina Kristo ndani yake, ni isiyo na nguvu. Lakini dini yoyote ambayo ndani yake ina Kristo iko chini ya damu yake mwenyewe na ina nguvu ndani yake. Mungu anachukia dini isiyo na nguvu. Lazima iwe na nguvu ndani yake. Lazima iwe na unyoofu ndani yake. Unyoofu unaleta nguvu. Unyoofu unaleta kuabudu halisi, sio mfano kawaida/mazoea, lakini nguvu za kikweli za ibada, kujua kwamba umevuka toka mautini kuingia uzimani (Yohana 5:24).

Napenda ninyi mlipate hili sasa. Kanisa linapaswa kujiinua lenyewe katika nguvu za Mungu. Kwa namna gani? Tuko karibu na mwisho sasa naamini Kanisa liko kwenye hali ambayo tunaweza kulifundisha vitu vya kindani, na kutoa nje, huku kujifanya kuamini na kuja kwenye kitu ambacho ni halisi. Unaona? Inabidi iwe ni kitu ambacho unajua.

Na hivyo mtu anapoishi kwa Imani na anatembea kwa imani, namaanisha imani bayana, yeye ametengwa kutoka kwenye dunia yote na kuwa kiumbe kipya ndani ya Kristo. Pale, sasa unaelekea kuwa sehemu ya Bibi Arusi. Unaona.? Unaingia kwenye hali ya kunyakuliwa sasa. Hiyo inamaanisha kwa kila mmoja wetu, sio Mchungaji tu, Mashemasi, na Wadhamini, hiyo inamaanisha washirika, kila mtu binafsi anatembea katika ulimwengu akiwa na mungu peke yake. Umebatizwa katika ufalme, na hakuna hata mmoja pale bali ni wewe na Mungu. Unaona?

Anatoa amri nawe unazitekeleza. Chochote anachosema, hakuna kivuli cha wasiwasi, unatembea sawa sawa mbele. Kama Bwana akisema hili, hakuna hata mtu duniani awezaye kukuzungumzia akutoe katika hilo, unaendelea mbele kwa usahihi. Sasa unakuja kwenye imani kamilifu. Kamilifu ya ukamilifu ambayo haiwezi kushindwa.

Nukuu za Kiingereza.
"Kutoka wakati ule" (61-0520) Aya 80 "Jinyenyekeshe uk. 10-11.
"Maji yasiyokoma yatokayo Mwambani" Aya 147, 150-153, 157, 160. Uungu wa yesu kristo (49-1225) Para. 80 "ufufuko wa Lazaro" (51-0729). Aya 37. Roho mtakatifu ametolewa kwa nini uk. 14-15, ufunuo kitabu cha mifano uk. 13, Ndipo Yesu akaja (57-1213), Para 23 Jehovah atajipatia (59-0417), Aya 84 umoja, Aya 186-189 "Israel na Kanisa sehemu 2" Aya 185-186, muhuri ya Pasaka uk. 35. Kanisa la wakati wa Laodikia CAB UK. 363 kutambua siku yako na ujumbe wake aya 192. vitu vyote ndani ya kristo Aya 68-71, Imani kamilifu Aya 39, 41, 114.

---

Jiwe la kujengea la Kiroho no. 99. Kutoka Neno lililofunuliwa la saa hii. Yamekusanywa na: Gerd Rodewald, Friendenstr. 69, D-75328 Schomberg, Germany Phone: (+49) 7235613, Fax (+49) 72353306

---

Anakuja mmoja na ujumbe ambao utatoka moja kwa moja kwenye Biblia, na kazi ya haraka itaizunguka dunia, mbegu zitaandikwa magazetini, vitu vya kusomea mpaka kila mbegu ya Mungu iliyokusudiwa imesikia.
[Ndugu Branham Mwenendo – utaratibu – mafundisho uk. 724].

*Kwa nakala zaidi za kiingereza au kiswahili Andika kwa:*

*Charles E. Y. Kanju,*
*Box 553 Korogwe - Tanga*
*E-mail: Chaelika@livel.com*
*Cellphone: 0784 704299/ 0718230098*